

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

12/07/2021

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKALLA ARUHUSU BIASHARA SOKO DOGO LA KARIAKOO.

-Ataka Barabara zote za kuingia Soko la Kariakoo zibaki wazi.

-Wafanyabiashara wa Shimoni washauriwa kuhamia Soko la Kisutu na Machinga Complex na amewapa ofa ya kutolipa Ushuru kwa miezi miwili.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Amos Makalla ameruhusu kuanza kwa shughuli za biashara Kwenye Soko dogo la Kariakoo Kutokana na eneo hilo kutoathiriwa na Moto.

RC Makalla amesema hayo alipotembelea sokoni hapo ambapo ametaka Wafanyabiashara wote wanaoendesha biashara zao eneo la hifadhi ya Barabara ya kuingia sokoni humo waondoke ili Barabara ibaki wazi.

Aidha RC Makalla amesema kwa wakati huu ambao hali ya usalama Soko kubwa haijaka sawa anashauri wafanyabiashara wachukuwe Mali zao na kuhamia Soko la Kisutu na Machinga Complex hadi marekebisho yatakapofanyika.

Kuhusu Soko la Shimoni ambalo inaelezwa halijaathiriwa kwa kiasi kikubwa na moto RC Makalla amesema Kutokana na Mfumo wa umeme sokoni humo kuharibika ameagiza ufanyike uratibu Wafanyabiashara wakachukue bidhaa zao na kuhamia Soko la Machinga Complex na Kisutu.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM